# ARUSHA MEAT COMPANY LTD.

P.O.BOX 14167

TANZANIA

TEL: +255272970304

Mob: +255734026767

E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

AMCL/TND/110/14 16/10/2025

# TANGAZO LA ZABUNI

Arusha Meat Company Limited (AMCL), ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma za uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Arusha Meat Company Limited inakaribisha maombi ya zabuni kutoka kwa **wataalamu binafsi** au **kampuni zilizobobea katika masuala ya kodi** kwa ajili ya kutoa huduma za **Ushauri wa Kikodi** kwa kipindi cha mwaka mmoja "2025/2026".

## MAJUKUMU YA MTALAM MSHAURI WA KIKODI

1. Kutoa ushauri wa kisheria na kitaalam kuhusu masuala ya kodi (VAT, PAYE, Withholding Tax, SDL, Corporate Tax n.k.)
2. Kukagua mifumo ya uwasilishaji wa ritani za kodi.
3. Kutoa mwongozo kwa kuzingatia mabadiliko ya sheria za kodi.
4. Kuwakilisha kampuni katika mawasiliano ya kikodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
5. Kushauri mbinu za kupunguza hatari na gharama za kikodi kisheria.
6. Kutoa mafunzo kwa idara ya fedha kuhusu utekelezaji wa sheria mpya za kodi.

## SIFA ZA WAOMBAJI

1. Awe **amesajiliwa kisheria nchini Tanzania** na kuwa na hati ya usajili wa biashara.
2. Awe na **leseni halali ya kutoa huduma za ushauri wa kikodi**.
3. Awe na angalau **wataalamu wawili (2)** waliobobea katika kodi, walio na usajili wa NBAA au TRA kama "Tax Practitioners".
4. Awe amehudumia angalau taasisi/kampuni tatu (3) kwa kazi zinazofanana katika kipindi cha miaka mitatu au zaidi.
5. Awe na TIN na cheti cha kuthibitisha ulipaji kodi (Tax Clearance Certificate).
6. Awe na uwezo wa kuwasilisha ushauri wa kifedha kwa kampuni.

NB: Waombaji wanatakiwa kufika katika Ofisi ya Idara ya Manunuzi na Ugavi, Arusha Meat Company Ltd-Sakina kuanzia tarehe 16 Oktoba 2025 hadi siku ya Tarehe 31 oktoba 2025 siku za kazi, kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni, kwa ajili ya kuchukua nyaraka rasmi za zabuni.

Tarehe ya mwisho ya kukabidhi zabuni ni 31 Oktoba 2025, saa 04:00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa rasmi tarehe 31 Oktoba 2025, saa 04:01 Asubuhi mbele ya waombaji au wawakilishi wao.

Nyote mnakaribishwa.

..........................................

**JONAS E. AYO**
**KAIMU MENEJA MKUU**
**ARUSHA MEAT COMPANY LIMITED**

MANAGER * ARUSHA MEAT COMPANY LIMITED P.O. Box 14167 ARUSHA - TANZANIA